

Jinsi ya Kujiepusha na Ponografia

Ayubu alisema: “Nimefanya agano [mkataba au mapatano] pamoja na macho yangu. Basi nawezaje kukaza fikira kwa bikira?” (Ayubu 31 : 1) Ni wazi kwamba Ayubu aliamua *mapema* jambo ambalo angefanya ikiwa angeshawishiwa. Unaweza kufanya hivyo kuhusu ponografia. Siri ni kujitayarisha mapema.

1

TAMBUA KILE UTAKACHOFANYA

Ni hali zipi zinazoweza kukufanya ukutane na ponografia kwenye Intaneti?

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Orodhesha mambo mawili unayoweza kufanya ili *upunguze* uwezekano wa kukutana na ponografia kwenye Intaneti.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

(Baadhi ya mambo ya kufikiria: wakati, mahali, kompyuta yako, maneno unayoingiza unapotafuta kitu kwenye Intaneti, watu unaoshirikiana nao kwenye mtandao.)



2

TAMBUA VIWANGO VYAKO VYA MAADILI

Alipokabili kishawishi cha kufanya uzinzi, Yosefu alikataa kwa uthabiti na kusema hivi: *“Ninawezaje kufanya ubaya huu mkubwa?”* (Mwanzo 39:9) Maneno *“Ninawezaje”* yanaonyesha kwamba Yosefu alikuwa na *viwango vya juu vya maadili*. Wewe pia unaweza kusitawisha viwango vya juu vya maadili. Ili kukusaidia kufanya hivyo, andika maoni yako kuhusu mambo yafuatayo.

Orodhesha sababu tatu kwa nini unaona kwamba ponografia ni mbaya.

1

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

2

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

3

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

(Baadhi ya mambo ya kufikiria: jinsi ponografia inavyomwathiri anayeitazama, jinsi inavyowadhalilisha wale wanaotumiwa katika ponografia, jinsi watengenezaji wa ponografia wanavyowatumia vibaya wale wanaotazama ponografia na kujifaidi kifedha kutokana nao, jinsi ndoa na familia zinavyoweza kuathiriwa.)

KUMBUKA: Mistari ya rangi nyeupe inayochorwa kwenye barabara kuu inatoa mwongozo, lakini *haitakufanya* uwe dereva mzuri. Vivyo hivyo, sheria zinazokuzuia usitazame ponografia zinaweza kukuongoza kwenye njia sahihi, lakini *hazitakufanya* uwe mtu mwadilifu. Hii ni sababu nzuri ya kukufanya ujivekee viwango vya juu vya maadili.

3

ANDIKA HATUA UTAKAZOCHUKUA

Ili kupunguza uwezekano wa kukutana na ponografia kwenye mtandao, nitafanya hivi . . .

.....

.....

.....

Nikikutana na ponografia ninapotumia Intaneti, nitafanya hivi . . .

.....

.....

.....

“Uyafanye macho yangu yapite ili yasione jambo lisilofaa.”—Zaburi 119:37.